**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

*Unapojibu tafadhali taja*:
Kumb: Na. AB.215/223/01/65 **2 Aprili, 2025**

**FURSA YA KUTOA HUDUMA YA KUSAFISHA MAZAO YA MIKUNDE NA UFUTA**

**Kwa: WATOA HUDUMA WOTE**

**UTANGULIZI**

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (Cereals and Other Produce Regulatory Authority – COPRA) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula Sura ya 249. Miongoni mwa majukumu yake ni kuandaa na kusimamia viwango endelevu vya uzalishaji, uchakataji, uhifadhi na masoko; kuandaa kanuni zinazosimamia uzalishaji, uchakataji, uhifadhi na masoko; na kusajili wafanyabiashara na majengo yanayohusika na sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko.

COPRA inatafuta watoa huduma wanaotambulika walio na mitambo ya kusafisha mazao ya nafaka na mikunde ili wapewe kazi ya kusafisha mazao hayo kwa lengo la kudhibiti ubora, usalama na viwango vinavyohitajika. Watoa huduma wote wenye nia na sifa wanaalikwa kutuma maombi na uthibitisho wa uwepo wa vifaa hivyo kwa ajili ya kutoa huduma hiyo kwenye ghala zilizosajiliwa na kupata leseni nchini.

Mamlaka itafanya tathmini ya maombi yatakayo wasilishwa na kuandaa orodha ya watoa huduma waliokidhi vigezo na kutangazwa. Watoa huduma hao watakaotangazwa wataruhusiwa kupewa tenda na waendesha Ghala wakati wa msimu wa biashara ya nafaka na mikunde ili kusafisha na kuchambua mazao hayo kama ilivyoainishwa na Mwongozo wa Biashara ya Dengu, Mbaazi, Choroko, Soya na Ufuta kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na Minada ya Kidijitali toleo la tatu 3 mwaka 2025.

**KAZI ZITAKAZOFANYIKA (WIGO WA KAZI)**

Miongoni mwa kazi zitakazofanyika katika kituo cha kusafisha mazao ni:

i. Kusafisha nafaka, mikunde na mbegu za mafuta kwa kuondoa uchafu, vumbi, mawe, takataka, na vitu vingine visivyohitajika.
ii. Kutumia teknolojia bora ya kusafisha na vifaa vya kisasa vinavyokidhi viwango vya usafi na ubora wa mazao husika.

*Jengo la Kahawa Plaza, Mtaa wa Njedengwa, S.L.P 2780, Dodoma -Tanzania.*
*Simu: +255 26 2310225, Barua pepe: info@copra.go.tz.*

iii. Kuzingatia kanuni za usalama wa chakula na viwango vya ubora wa mazao husika.
iv. Kutoa taarifa mara kwa mara mamlaka husika juu ya taratibu za usafishaji na ukaguzi wa ubora.
v. Kufanya Matengenezo ya mashine na vifaa vya kusafisha kwa wakati.
vi. Kuwajengea uwezo waendesha ghala kuhusu sifa za ubora wa nafaka na mikunde.

**VIGEZO/SIFA ZA KUCHAGULIWA**

Watoa huduma wenye nia lazima watimize vigezo vifuatavyo:

1. **Kutambulika:** Kampuni iliyosajiliwa ndani ya nchi au kimataifa, Chama cha Ushirika au Taasisi iliyosajiliwa na mamlaka husika.
2. **Uzoefu:** Uzoefu wa kutoa huduma ya kusafisha nafaka na mikunde au bidhaa zinazoendana na mazao hayo.
3. **Kufikia Ubora unaohitajika:** Uwezo wa kufikia viwango vya ubora wa juu, kama ilivyoainishwa katika miongozo ya Biashara na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na viwango vingine vya Kikanda na Kimataifa.
4. **Uwezo wa Kiufundi:** Kuwa na vifaa muhimu vya kiufundi, miundombinu na wafanyikazi wenye ujuzi na taarifa muhimu za uwezo wa vifaa husika.
5. **Uzingatiaji:** Uwezo wa kuzingatia mahitaji yote ya udhibiti ubora, ikiwa ni pamoja na viwango vya afya na usalama.

**MAHITAJI MUHIMU WAKATI WA KUTUMA MAOMBI**

Watoa huduma lazima wawasilishe nyaraka zifuatazo kama sehemu ya kuonesha nia:

1. Maelezo ya kina ya kampuni, Chama cha Ushirika au Taasisi ikijumuisha miaka ya uzoefu na umahiri wa kazi hiyo.
2. Maelezo ya teknolojia, vifaa na mbinu zitakazotumika kusafisha mazao.
3. Orodha ya miradi iliyotekelezwa (ikiwa umewahi fanya kazi hiyo), ikijumuisha aina ya nafaka/mikunde iliyosafishwa, kiasi na ukubwa wa kazi.
4. Nakala za vyeti usajili mwombaji, TIN, leseni ya biashara na vibali vingine husika (kama vipo) vya kazi husika.
5. Anuani za angalau taasisi au watu wawili uliowahi kuwafanyia kazi.
6. Mapendekezo ya gharama (bei) au ada utakayotoza kwa huduma za kusafisha mazao.
7. Uthibitisho wa kufuata viwango vya usalama wa chakula na ubora itakuwa sifa ya ziada/nyongeza.
8. Utayari wa kuanza kazi (Muda utakaotumia kuweka mitambo na kuanza kazi).
9. Onyesha mikoa ambayo unapendelea kufanya kazi ndani ya Tanzania.

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI**

Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe: info@copra.go.tz mwisho wa kutuma maombi hayo ni tarehe 11 Aprili, 2025 kabla ya saa 5:59 usiku

**VIGEZO WAKATI WA TATHMINI**

Maombi yote yatatathiminiwa kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

i. Uzoefu na utaalamu wa kusafisha nafaka na mikunde.
ii. Mifumo ya kudhibiti ubora na uwezo wa mitambo uliyonayo.
iii. Uwezo wa kukidhi kiasi na muda wa usafishaji.
iv. Ufanisi wa gharama na thamani ya fedha.
v. Uzingatiaji wa Sheria, kanuni na taratibu za sekta.

**USIRI**

Taarifa zote zitakazotolewa na mtoa huduma zitakuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kiofisi pekee na zitahifadhiwa kwa siri.

Irene M. Mlola
**MKURUGENZI MKUU**